



NAETISL

National Association of
Educational Translators and
Interpreters of Spoken Languages



MODDC

Missouri
Developmental
Disabilities Council

Kuhitimu kwa Wanafunzi wenye Ulemavu: Mwongozo wa Mzazi

Funding for the Supporting Language Access in Schools Project in Missouri provided by the Missouri Developmental Disabilities Council, was supported by the Administration for Community Living (ACL), U.S. Department of Health and Human Services (HHS) as part of a financial assistance award totaling \$1,361,246 with 100 percent funding by ACL/HHS. The contents are those of the author(s) and do not necessarily represent the official views of, nor an endorsement, by ACL/HHS, or the U.S. Government.



naetisl@gmail.com

NAETISL



Follow us



MODDC



moddc@moddcouncil.org



www.naetisl.org

www.moddcouncil.org





Kuhitimu kwa Wanafunzi wenye Ulemavu: Mwongozo wa Mzazi

Je, wanafunzi wenye ulemavu wanapaswa kukidhi mahitaji ya kuhitimu sawa na wanafunzi wengine?

Sio kila wakati. Graduation requirements for students with disabilities may be adjusted to meet their individual needs. While some students earn a standard diploma, others may follow a modified path that still allows them to complete high school successfully.

Nini kinaamua jinsi mwanafunzi mwenye ulemavu atahitimu?

Timu ya Mpango wa Elimu ya Kibinafsi (IEP) huamua njia ya mwanafunzi hadi kuhitimu. Uamuzi huu unatokana na:

- Uwezo wa mwanafunzi, mahitaji yake na malengo yake ya baada ya shule ya sekondari
- Aina na ukali wa ulemavu
- Maendeleo ya viwango vya kitaaluma na malengo ya IEP

Ni aina gani za diploma au chaguzi za kuondoka zinazopatikana?

Chaguzi za kuhitimu ni tofauti kulingana na majimbo, lakini mara nyingi hujumuisha :

- Diploma ya Kawaida
- Mwanafunzi anakidhi mahitaji yote ya elimu ya jumla, ikiwezekana na marekebisho.
- Diploma iliyorekebishwa ama Cheti cha Kukamilisha
- Mwanafunzi hukamilisha kosi kulingana na viwango vilivyorekebishwa, mara nyingi vinavyolengwa kulingana na IEP yao. Hizi zinaweza zisifikie mahitaji ya kuingia chuo kikuu lakini bado zinaonyesha mafanikio.





- IEP au Diploma Mbadala
- Mwanafunzi anafikia malengo yaliyowekwa kwenye mpango wake wa IEP badala ya kosi ya kawaida. Njia hii ni ya wanafunzi wenye ulemavu mkubwa.
- Cheti cha Kuhudhuria ama Kukamilisha
- Hupeanwa wakati mwanafunzi hafikii mahitaji ya diploma lakini anamaliza programu yake ya IEP na kuhudhuria shule mpaka afikie miaka 21.

Nani anaamua ni chaguo gani la kuhitimu lililo bora zaidi?

Timu ya IEP, ikiwa na mchango wa mwanafunzi na familia, hufanya uamuzi huu. Kawaida, mipango haunza mwanafunzi akiwa kati ya miaka 14-16 kama sehemu ya huduma za mpito katika IEP. Ni muhimu kwa:

- Pitia chaguzi za kuhitimu mapema
- Kuelewa jinsi kila njia inavyoathiri fursa za siku zijazo
- Rudia uamuzi huo mara kwa mara wakati wa shule ya upili

Mwanafunzi anaweza kubadilisha njia za kuhitimu?

Ndio. Mipango ya kuhitimu inahitaji kuangaliwa tena angalau mara moja kila mwaka. Iwapo utendaji, malengo, au uwezo wa mwanafunzi utabadilika, timu ya IEP inaweza kurekebisha njia ya kuhitimu ipasavyo.

Ni nini athari za aina tofauti za diploma?

Kila chaguo linaweza kuathiri mipango ya siku za usoni za mwanafunzi:

- Diploma ya kawaida

Kawaida inahitajika kwa chuo kikuu, jeshi, au ajira ya ushindani





- Diploma iloyorekebishwa ama ya IEP

Inaweza kukubaliwa na baadhi ya shule za ufundi au programu zinazoungwa mkono za ajira, lakini isifikie vigezo vya kawaida vya kujiunga na chuo

- Cheti cha kuhudhuria/ kukamilisha

Inatambua juhudi na ukuaji lakini hailingani na diploma

Wazazi wanawezaje kumsaidia mtoto wao kupitia mchakato huu?

Uko na jukumu kubwa sana kumsaidia mtoto wako kufaulu. Unaweza:

- Kuuliza shule ikuelezee chaguo zote za diploma na za kutoka
- Kumhimiza mtoto wako kusema malengo yake ya siku za usoni
- Kumsaidia mtoto wako kutambua mambo anayopenda kazini, chuo kikuu, au mafunzo
- Kuudhuria na kushiriki katika mikutano yote ya IEP na ya mpito
- Kuhakikisha mpango wa kuhitimu unapatana na uwezo na malengo ya muda mrefu ya mtoto wako

Nini kitafanyika ikiwa mtoto wangu atabaki shuleni baada ya miaka 18?

Wanafunzi wenye ulemavu wana haki ya kupata huduma za elimu maalum kufikia umri wa miaka 21 (au hadi wapate diploma, chochote kitakachotangulia). Iwapo mtoto wako anahitaji muda zaidi ili kukuza ujuzi wa kitaaluma, ufundi stadi au maisha, anaweza kuendelea kupata usaidizi hata baada ya wenzao kuhitimu.

Nawezaje kupata usaidizi katika lugha yangu?

Omba huduma za mkalimani katika shule ya mtoto wako ama katika ofisi za Wilaya ya shule. Omba taarifa zilizotafsiriwa na kuandikwa iwapo unazihitaji. Taarifa zinazopeanwa kwa wazazi wote katika wilaya ya shule zinafaa kupatikana kwako pia.





Vidokezo kwa familia

- Usiogope kuuliza maswali!
- Omba shule ieleze jinsi maamuzi ya kuhitimu hufanywa na jinsi maamuzi hayo yanavyoathiri wakati ujao wa mtoto wako

Kuhitimu kunapaswa kuonyesha maendeleo na uwezo wa mtoto wako binafsi. Safari ya kila mwanafunzi ni ya kipekee, na lengo ni mtoto wako aache shule ya upili akiwa na ujuzi, ujasiri, na usaidizi anaohitaji ili kusonga mbele.

